# TIST

## MPWAPWA KONGWA,GAIRO HABARI MOTO MOTO ©

Tel. +255748-466545/537720 , P.O.BOX 6049 MOROGORO E-Mail info@ tist.org
JUNI, 2006

**Kikundi cha Ushirikeli**

Kikundi cha Ushirikeli kinapatikana katika kijiji cha Idilo umbali wa kilomita nne magharibi mwa mji wa Mpwapwa. Kikundi hiki kilianzishwa tarehe 15/01/2003 chini ya mradi wa TIST kikiwa na wanachama sita wakiwa na malengo yafuatayo;- kuzuia uharibifu wa mazingira na kuyaboresha hasa kwa kupanda miti katika kijiji chao, kupiga vita dhidi ya maradhi yanayoisumbua jamii kuweka mazingira safi, kupiga vita dhidi ya janga la ukimwi na magonjwa yanayoambatann nao kwa kuto mafunzo kwa jamii ya Wanaidilo na kuboresha maendeleo ya akina mama na watoto wao katika kijiji cha idilo na maeneo yanayozunguka

Kwa sasa kikundi cha Ushirikeli kina wanachama 16 na sasa kinategemea kujisajili kama CBO katika halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa. Pia kikundi kimefanikiwa kuyabadilisha mazingira ya ukame ya kijiji kuwa katika hali inayopendeza machoni mwa watu. Kwa ajili ya hiyo kimeandaa katiba na nembo ya kikundi ambayo huelezea maana halisi ya neno ushirikeli kuwa ni uwezo wa mtu mwingine kuona matatizo yanayowakabili watu wengine na kusaidiana nao katika kuyatatua matatizo hayo. Wanakikundi cha ushirikeli wanashauri wanajamii wote wajiunge pamoja katika kuifanya dunia kuwa ni mahali panapopendwa na viumbe vyote

**Kilimo**

**Uvunaji na utunzaji wa mazao**

Sasa msimu wa kuvuna mazao ndio umewadia. Kutokana na upungufu mkubwa wa mvua katika maeneo yote ya mkoa wa Dodoma hata mavuno mwaka huu si mazuri sana. Wanavikundi wanatakiwa kuwashauri wanakijiji wengine kuwa makini katika utunzaji wa chakula kidogo kilichopatikana. Pia tunatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ili kukabiliana na kippindi hiki kigumu;-

**Tuhifadhi chakula tulichopata katika maghala**

Tunatakiwa kuhifadhi chakula katika maghala kwa ajili yetu ili kuwe na chakula cha kutosha wakati bei za vyakula zitakapopanda hapo baadaye. Kama kuna uwezekano wa kununua chakula kwa ajili ya ziada basi tununue mapema na kuhifadhi ili kukabiliana na ongezeko la bei linalotazamiwa kutokea hapo baadaye. Pia tuepuke kuuza kwa wachuuzi mazao yetu kidogo tuliyoyapata.

**Kupunguza matumizi yasiyo ya lazima**
Wanakijiji mnatakiwa kuwa makini katika matumizi ya chakula kidogo kilichopatikna kwa kuepuka kufanya matumizi yasiyo ya lazima kama vile kupikia pombe, sherehe zisizo na ulazima wowote nk. Hii itasaidia chakula kilichopatikana kukaa kwa muda mrefu.

**Kuanzisha miradi mbadala kwa ajili ya kujiongezea kipato**

Tunatakiwa kuwa wabunifu katika kuanzisha miradi mbalimbali ambayo itatusaidia kuacha kuuza mazao kwa wachuuzi. Tunaweza pia kujishughulisha na biashara ndogondogo ili kupunguza ukali wa maisha na kujipatia matumizi madogomadogo. Akina baba wasiwaachie wanawake peke yao katika kutafuta chakula na kupoteza muda katika vilabu vya pombe. Familia ziungane kwa pamoja ili kutafuta kwa pamoja.

**Kupunguza idadi ya mifugo**

Tunatakiwa kuwa na mifugo ile ambayo tutamudu kuihudumia kwa kipindi chote bila kuathiri mazingira yanayotuzunguka. Kwa wale wenye idadi kubwa ya mifugo na kuonyesha kutokuimudu wanatakiwa kuiuza na kununua chakula na matumizi mengine ya kila siku ikiwa wataona inawezekana. Pia tunatakiwa kuiboresha mifugo tuliyonayo ili kuweza kujipatia lishe na matumizi mengine kutokana na mazao ya mifugo hiyo kama maziwa, mbolea nk

**Kutunza vyanzo vya maji vilivyopo**

Tujitahidi kuvitumia kwa uangalifu mkubwa vyanzo vya maji vilivyopo kwani kutokana na upungufu wa mvua mwaka huu tunaweza tukapatwa na janga la ukame. Pia tunaweza kutumia maji yaliyopo kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ili kujipatia kipato. Hatutakiwi kukata miti ovyo katika vyanzo vya maji kwa sababu kama tukikata vyanzo vyote vitakauka na kusababisha kukosa maji kabisa. Mifugo itengewe maeneo maalum kwa ajili ya kunywesha mbali na maji yanayotumika kwa matumizi ya binadamu.

## VIRUSI NA UKIMWI

**Jinsi wanavikundi wa TIST wanavyoweza kuzuia kuenea kwa ukimwi**
Janga la Ukimwi limekuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo katika jamii ya watanzania. Katika maeneo ya vijijini ambako kwa asilimia kubwa hali ya maisha huwa ni ngumu ukimwi umeyageuza maeneo hayo kuwa mahali pasipofaa kuishi kitu ambacho si kweli ikiwa sote kwa pamoja tutaungana kuupinga kwa nguvu zote. Ukimwi umekuwa ukienea kwa kasi kubwa katika jamii ya watanzania. Hii ni kwa sababu wengi wetu hatuna maamuzi yaliyo sahihi mara tutakiwapo kutoa maamuzi hayo. Hapa chini kuna baadhi ya mambo muhimu ambayo ikiwa wanavikundi wa TIST watayafuata kwa makini na kuyatekeleza basi watasaidia kuokoa wanakijiji wengine.

**Thamini ndoto zako**
Kila mtu ana malengo yake katika maisha yake ya baadaye. Pia katika malengo hayo kuna mipango ambayo anaifanya ili kufikia malengo hayo. Tunahitaji kuwa waangalifu na kuishi kwa makini zaidi ili yale tuliyoyapanga yaweze kufikia. Kamwe tusikubali yale tuliyojipangia yakatishwe na ukimwi na pia tusikubali starehe za muda mfupi ziharibu ndoto zetu za baadaye

**Zitambue hatari na athari za ukimwi kabla ya kufanya mapenzi kiholela**
Watu wanapofanya tendo la ndoa kiholela huwa katika hatari kubwa ya kupata maambukizi. Hii ni kwa sababu tendo hufanywa kwa kuibia katika mazingira yasiyoruhusu hivyo si rahisi kwa wahusika kufuata njia za kujikinga na maambukizi. Hatari hizo ni pamoja na kutokutafiti mienendo yao wote wawili. Hivyo maamuzi yao mabaya yanaweza kusababisha mateso kwa watoto watakaobaki ikiwa watu hawa watakufa kwa ukimwi

**Epuka kujaribu au kufanya mambo kabla ya kuyafanyia uchunguzi wa kina**
Baadhi ya watu hasa vijana hupenda kujaribu kila kitu wanachoona kikifanywa na watu wengine au kukisikia bila kufanyia uchunguzi wa kina madhara ya mambo hayo wanayoyaiga. Wanavikundi wa TIST wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kufundisha rika hili la vijana kuacha kuiga mambo ambayo hayana manufaa yoyote katika jamii zao

**Toa elimu kwa jamii ihusuyo madhara ya ukimwi katika maendeleo yao binafsi na ya taifa**
Kazi mojawapo ya vikundi vya TIST ni kutoa elimu ihusuyo maambukizi ya ukimwi kwa jamii inayowazunguka. Hivyo ni muhimu kwa wanavikundi kuandaa mkakati maalum kwa ajili ya kutoa elimu ya ukimwi katika vijiji vyetu. Mnaweza kutenga siku maalum kwa ajili ya kufanya mafundisho hayo ambayo mwaweza kuyafanya kwa maigizo, nyimbo au katikas mikutano ya hadhara. Pia tunaweza kutumia taasisi nyingine kama makanisa na shule

**Tumia muda wako kujisomea vijitabu na masomo mbalimbali yahusuyo kujikinga na maambukizi ya ukimwi**
Tunapaswa kutumia muda mwingi katika kujisomea majarida mbalimbali ili tuwe na uzoefu katika kufundisha jamii kuhusu madhara ya ukimwi. Hatutakiwi kuwa wababaishaji katika mafundisho tuyatoayo kwa jamii. Pia tukijisomea tutakuwa na uwezo wa kufahamu vizuri jinsi ya kujikinga na ukimwi

**Kuwa muwazi, (jifunze kutoa hisia zako kwa jamii)**
Kila mwanajamii ana haki ya kutoa kile anachofikiri kuwa ni sahihi. Kwa hiyo usiwe na woga kutoa mawazo yako kwa jamii kwani mawazo yako yanaweza kuibadilisha jamii kuelekea katika mstari ulionyooka kwa kuacha yale yasiyofaa katika kudhibiti ukimwi

**Epuka kukaa na makundi yenye muelekeo mbaya kwa muda mrefu**
Tunapaswa kuepuka makundi mabaya ambayo tunadhani hatutaweza kujizuia kuiga na kuyafanya yale mambo yanayoonyesha kuvunjika kwa maadili kutoka kwao. Ikiwa tutalazimika kuwa nao tunapaswa kufanya kila liwezekanalo kuwafanya wao waige muelekeo wetu.

**Uwe mwaminifu kwa mwenza na marafiki wanaokuzunguka**
Uaminifu ni suala la msingi katika jamii yoyote ili kuleta maendeleo ya jamii hiyo. Kama wanavikundi wa TIST watakuwa waaminifu katika familia zao na katika jamii inayowazunguka watawezesha watu wanaowazunguka kujenga uaminifu kwao kwani watakuwa wanajifunza kupitia matendo yao mema. WanaTIST wanatakiwa wawekielelezo kizuri katika jamii zao kwa kufanya kazi kwa bidii, na kutoa mafunzo yahusuyo maadili mema katika vijiji vyao

**Shikilia maadili ya dini yako**
Ikiwa wanavikundi watafuata maagizo ya dini zao kwa uaminifu mkubwa waatasaidia kupungua athari za kuenea kwa ukimwi. Hakuna dini hata moja inayoruhusu watu kufanya tendo la ndoa bila kufunga ndoa. Kama kuna wanavikundi ambao ni viongozi wa makanisa wanapaswa kuwahimiza waumini wao kuacha tabia ambazo ni kinyume na maagizo ya dini zao kama vile kutumia sigara, madawa ya kulevya, uzinzi na mengine yanayofanana na hayo.

**Maagizo kwa wawezeshaji**
Wawezeshaji wanatakiwa kufanya mambo yafuatayo katika maeneo yanayowazunguka.

- Kusimamia wanavikundi katika eneo lake katika kuanzisha CBO na kuiandikisha katika halmashauri zao za wilaya.
- Wanatakiwa kuomba katika serikali za maeneo yao eneo kubwa la kupandia miti ya vikundi vyote. Wote watapanda miti katika eneo moja lakini kila kikundi nna miti yake
- Kufanya maandalizi ya vitalu vya miti, kuandaa mbegu. Kila eneo linatakiwa liwe na vitalu vyenye miti isiyopungua 50000
- Suala la posho za wawezeshaji bado linashughulikiwa na ofisi
- Kwa wale wanaotaka kuanzisha vikundi basi wanaruhusiwa kufanya hivyo ila tu wanatakiwa kufuata masharti ya mradi wa TIST

**Maagizo kwa wanavikundi**

- Vikundi vyote vyenye miti zaidi ya 1000 vitaendelea kupata malipo yao kama kawaida ila wanahimizwa kujiandaa kwa ajili ya kuongeza miti kwa msimu ujao.
- Kwa wale wenye miti chini ya 1000 wanatakiwa wajiandae ili mwaka huu waongeze miti yao ifike zaidi ya 1000 ili waendelee kupata malipo yao
- Wakaguzi wa miti wataanza kukagua na kuhesabu miti kuanzia mwezi wa saba. Hivyo endeleeni kuitunza miti yenu kwa kuipalilia na kuzuia wanyama wasiiharibu. Kumbukeni kuwa miti illiyo katika maeneo machafu hayatahesabiwa kwa ajili ya usalam awa miti na wakaguzi.
- Tunategemea kuwanufaisha wale wenye majiko banifu hivyo mnatakiwa kuyatengeneza kwa wingi ili wanavikundi wanufaike zaidi.

**Takwimu za TIST za hivi karibuni**

| | |
|---|---|
| Idadi ya vikundi | 229 |
| Idadi ya miti | 171646 |
| Idadi ya miche | 10008 |
| Idadi ya node | 7 |

**Ratiba ya mikutano ya node**

| Julai 2006 | Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa | Jumamosi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wiki la 2<br>Tarehe 9 –15 | - | Igovu | Bumila | - | Mbori | Tambi -<br>Igunga |
| Wiki la 3<br>Tarehe 16 –22 | Chamkoloma | - | Matongoro | - | Majawanga | |